SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 21 JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) NOVEMBA 2022

NITAENDELEZA MIPANGO ILIYOANZISHWA NA WATANGULIZI WANGU: WAZIRI KAIRUKI

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki (Mb) akizungumza na watumishi wa Ofisi hiyo pamoja na Taasisi zilizo chini ya Ofisi hiyo wakati wa hafla ya kumkaribisha baada ya kuteuliwa kuwa Waziri katika ofisi hiyo. Pichani, katikati ni aliyekuwa Waziri wa OR – TAMISEMI ambaye kwa sasa ni Waziri wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mhe. Innocent Bashungwa ambaye naye alikuwa anaagwa na watumishi wa OR – TAMISEMI. Upande wa kulia ni Naibu Waziri wa OR – TAMISEMI anayeshughulikia Elimu, David Silinde (mwenye suti ya bluu).

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania

KARIBU SANA MHE. ANGELLAH JASMINE KAIRUKI

Mapema mwezi Oktoba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan alifanya mabadiliko madogo ya Baraza la Mawaziri ambapo alimteua Mhe. Angellah Jasmine Kairuki kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) kuchukua nafasi ya Mhe. Innocent Bashungwa ambaye alihamishiwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Wakati akizungumza na Watumishi wa Ofisi ya Rais TAMISEMI na Taasisi zilizo chini ya TAMISEMI waziri kairuki alisema kuwa ataendeleza mipango yote iliyoanzishwa na Mawaziri waliomtangulia katika ofisi hiyo ili kuhakikisha Serikali inakamilisha mipango yake ya Maendeleo kwa kasi zaidi.

Tunampongeza sana Waziri Kairuki kwa kuaminiwa na Mhe. Rais Samia hadi kuteuliwa kuongoza ofisi hiyo muhimu. Matarajio yetu ni kwamba mipango yote mizuri iliyokuwa inaendelea kutekelezwa ataendelea kuisimamia kwa kasi zaidi.

Walimu wanatarajia kuwa Waziri kairuki ataendelea kusimamia maslahi yao ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kiradi yote ya Elimu inayotekelezwa katika ngazi ya shule na halmashauri itakamilika kama ilivyopangwa ili kuendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa walimu.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) inamkaribisha sana Waziri Kairuki na inaahidi kumpatia ushirikiano wa kila namna ili aweze kutekeleza majukumu yake kwa urahisi zaidi. Karibu sana Mhe. Angellah Jasmine Kairuki tuendelee kuwahudumia walimu wetu.

BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti
Paulina Nkwama

Wajumbe
Richard Odongo
Revocatus Misonge
Mectildis Kapinga
Lameck Mbeya
Zachary A. Dida

Mhariri Mkuu
Gerard Chami

Mhariri
Adili Mhina

Msanifu Kurasa
Lucas Gordon

KATUNI



OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI
WA WALIMU (TSC)

MATOKEO YA SENSA YA SITA TANZANIA SENSA 2022
MPANGO JUMUISHI KWA MAENDELEO ENDELEVU

IDADI YA
WATANZANIA
61,741,120

WANAWAKE:
31,687,990 (51%)

WANAUME:
30,053,130 (49%)

"Watu wote hawa kwa takwimu za makundi hayo, wanamtegemea Mwalimu katika kupambana na Maadui Wakubwa wa Maendeleo; Ujinga, Maradhi na Umaskini.
Kazi Iendelee

www.tsc.go.tz secretary@tsc.go.tz Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania

NITAENDELEZA MIPANGO ILIYOANZISHWA NA WATANGULIZI WANGU: WAZIRI KAIRUKI

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki (Mb) akisalimiana na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama wakati alipowasili katika ofisi za OR – TAMISEMI mji wa serikali Mtumba jijini Dodoma kwenye hafla ya kukaribishwa baada ya kuteuliwa kushika nafasi hiyo hivi karibuni.

Na Mwandishi Wetu – Dodoma.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki (Mb) amesema ataendeleza mipango yote iliyoanzishwa na Mawaziri waliomtangulia katika ofisi hiyo ili kuhakikisha Serikali inakamilisha mipango yake ya Maendeleo kwa kasi zaidi.

Waziri Kairuki amayasema hayo Oktoba 6, 2022 wakati akizungumza na Watumishi wa OR – TAMISEMI pamoja na Taasisi zilizo chini ya ofisi hiyo katika hafla ya kumkaribisha Waziri huyo na kumuaga aliyekuwa Waziri wa Wizara hiyo, Mhe. Innocent Bashungwa ambaye aliteuliwa kuwa Waziri wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Akizungumza katika hafla hiyo iliyofanyika katika ofisi za OR – TAMISEMI Mtumba, jijini Dodoma, Waziri Kairuki alisema kuwa Waziri Bashungwa na Mawaziri wengine waliomtangulia walifanya kazi nzuri na ndiyo maana miradi mingi ya Serikali imetekelezwa kwa ufanisi, hivyo anaamini kuwa mipango waliyoianzisha ni mizuri na yeye ataendelea kuiboresha ili kuleta mafanikio zaidi kwa wananchi .

"Ninatambua mawaziri waliotangulia wamefanya kazi kubwa katika Ofisi hii, na mimi ninawaahidi kuwa nitaendeleza mipango yote ambayo wenzangu waliianzisha kwa lengo la kuleta maendeleo kwa wananchi. Mimi sio mtu ambaye nikiingia ofisi mpya napangua kila kitu walichoanzisha wenzangu, ni

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki (Mb) (wa kwanza kushoto) akizungumza na watumishi wa Ofisi hiyo pamoja na Taasisi zilizo chini ya Ofisi hiyo wakati wa hafla ya kumkaribisha baada ya kuteuliwa kuwa Waziri katika ofisi hiyo. Hafla hiyo imefanyika Oktoba 6, 2022 katika ofisi za OR – TAMISEMI mji wa serikali Mtumba jijini Dodoma.

NITAENDELEZA MIPANGO ILIYOANZISHWA NA WATANGULIZI WANGU: WAZIRI KAIRUKI

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki (Mb) (katikati mstari wa mbele) akiwa katika picha ya pamoja na Naibu Waziri OR TAMISEMI anayeshughulikia Elimu, Mhe. David Silinde (Mb) (wa pili kutoka kushoto), Katibu Mkuu wa OR TAMISEMI, Prof. Riziki Shemdoe (wa pili kutoka kulia), Naibu Katibu Mkuu OR TAMISEMI anayeshughulikia Afya, Dkt. Grace Magembe (wa kwanza kutoka kulia), Naibu Katibu Mkuu OR – TAMISEMI anayeshughulikia Elimu, Dkt. Charles Msonde (wa kwanza kutoka kushoto) pamoja na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya OR – TAMISEMI wakati wa hafla ya kumkaribisha Waziri huyo iliyofanyika katika ofisi za OR – TAMISEMI mji wa serikali Mtumba jijini Dodoma Oktoba 6, 2022.

lazima tuwe na mwendelezo wa kile kilichoanzishwa ili tufikie malengo," alisema.

Kairuki aliongeza kuwa pamoja na kuwa OR – TAMISEMI ni Wizara kubwa, kazi yake ya kuiongoza itakuwa rahisi endapo viongozi na watumishi wa wizara hiyo watafanya kazi kwa bidii, weledi na ushirikiano mkubwa huku akionesha kuwa hatokubali mtu yeyote kumrudisha nyuma katika kusimamia utekelezaji wa kazi katika ofisi hiyo.

"Naelewa TAMISEMI ni Wizara kubwa na inawagusa wananchi moja kwa moja kupitia Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serilai za Mitaa. Hivyo, ninaamini kuwa tukiwa na ushirikiano mzuri kazi itakuwa rahisi, lakini kama kiongozi akisema hili wengine wanasema lile kazi itakuwa ngumu na hatutafikia malengo na mimi sitakubali kurudishwa nyuma," alisema.

Aliendelea kueleza kuwa anamshukuru Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumwamini na kumteua kuwa Mbunge na hatimaye Waziri katika Wizara hiyo huku akieleza kuwa ana uzoefu katika nafasi ya uwaziri ambapo ameongoza Wizara mbalimbli na hivyo atatumia uzoefu huo kutimiza malengo ya Serikali ya Awamu ya Sita ambayo imedhamiria kuboresha maisha ya wananchi.

Awali, Waziri wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mhe. Innocent Basungwa alimueleza Waziri Kairuki kuwa OR – TAMISEMI ina viongozi na

NITAENDELEZA MIPANGO ILIYOANZISHWA NA WATANGULIZI WANGU: WAZIRI KAIRUKI

watumishi wazuri ambao alifanya nao kazi kwa ushirikiano mkubwa katika kipindi chote alichokuwa Waziri wa OR – TAMISEMI na hivyo anaamini kuwa ushirikiano huo utaendelea kwa Waziri Kairuki.

Bashungwa aliwashukuru watumishi wote wa OR – TAMISEMI kwa kufanya nae kazi vizuri ambapo alisema utendaji mzuri wa watumishi hao ndio ambao umefanya Rais Samia Suluhu Hassan aendelee kumwamini na kuamua kumteua kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

"Ninawashukuru sana watumishi wote kwa ushirikiano mlionipa katika kipindi chote nilichokuwa hapa. Kazi nzuri mliyoifanya ndiyo iliyofanya na mimi nionekane kuwa ninafanya vizuri. Ninamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini na kuona bado ninafaa kuendelea kumsaidia katika Serikali yake. Ninawaomba ushirikiano na upendo mlionipa mumpatie pia Waziri Kairuki ili aweze kufanya kazi yake vizuri," alisema Bashungwa.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa OR – TAMISEMI, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya OR – TAMISEMI pamoja na watumishi wa Ofisi hiyo.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki (Mb) (katikati mstari wa mbele) akiwa katika picha ya pamoja na Naibu Waziri OR TAMISEMI anayeshughulikia Elimu, Mhe. David Silinde (Mb) (wa pili kutoka kushoto), Katibu Mkuu wa OR - TAMISEMI, Prof. Riziki Shemdoe (wa pili kutoka kulia), Naibu Katibu Mkuu OR TAMISEMI anayeshughulikia Afya, Dkt. Grace Magembe (wa kwanza kutoka kulia), Naibu Katibu Mkuu OR TAMISEMI anayeshughulikia Elimu, Dkt. Charles Msonde (wa kwanza kutoka kushoto) pamoja na baadhi ya Watumishi wa OR –TAMISEMI na watumishi wa Taasisi zilizo chini ya ofisi hiyo wakati wa hafla ya kumkaribisha Waziri huyo iliyofanyika katika ofisi za OR – TAMISEMI mji wa serikali Mtumba jijini Dodoma Oktoba 6, 2022.

Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mhe. Innocent Bashungwa (Mb) (kushoto) akipokea zawadi kutoka kwa Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Prof. Riziki Shemdoe kwenye hafla ya kumuaga Waziri huyo baada ya kuhamishwa kutoka OR – TAMISEMI kwenda Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Hafla ya kumuaga Waziri huyo ilifanyika katika ofisi za OR – TAMISEMI mji wa serikali Mtumba jijini Dodoma Oktoba 6, 2022.

Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mhe. Innocent Bashungwa (Mb) (kushoto) akiwaaga watumishi wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) (hawapo pichani) ambapo alikuwa Waziri wa OR – TAMISEMI kwa kipindi cha miezi tisa. Pembeni yake ni Naibu Waziri wa OR – TAMISEMI, Mhe. David Silinde, hafla ya kumuaga Waziri huyo ilifanyika katika ofisi za OR – TAMISEMI mji wa serikali Mtumba jijini Dodoma Oktoba 6, 2022.

Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mhe. Innocent Bashungwa (Mb) (wa kwanza kushoto) akiwaaga watumishi wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) ambapo alikuwa Waziri wa OR – TAMISEMI kwa kipindi cha miezi tisa. Hafla ya kumuaga Waziri huyo ilifanyika katika ofisi za OR – TAMISEMI mji wa serikali Mtumba jijini Dodoma Oktoba 6, 2022.

Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mhe. Innocent Bashungwa (Mb) akisalimiana na Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba mara alipowasili kwenye hafla ya kuagwa na watumishi wa OR TAMISEMI ambapo alikuwa waziri katika ofisi hiyo kabla ya kuhamishiwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mhe. Innocent Bashungwa (mb) akisalimiana na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama mara alipowasili kwenye hafla ya kuagwa na watumishi wa OR TAMISEMI ambapo alikuwa waziri katika ofisi hiyo kabla ya kuhamishiwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

TSC YAANIKA MAFANIKIO ILIYOYAPATA KATIKA SERIKALI YA AWAMU YA SITA

Na Mwandishi Wetu – Dodoma.

Tume ya Utumishi wa Walimu TSC imeeleza mafanikio mbalimbali yaliyopatikana katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita na kueleza mikakati yake ya mbeleni katika kutoa huduma bora kwa walimu.

Mafanikio hayo yamebainishwa Oktoba 27, 2022 na Katibu wa TSC, Paulina Nkwama wakati alipokutana na waandishi wa habari katika Ukumbi wa Idara ya Habari – MAELEZO jijini Dodoma ikiwa ni moja ya mikakati ya Serikali katika kutoa habari kwa wananchi juu ya shughuli zinazotekelezwa na Serikali.

Nkwama alianza kwa kueleza kuwa lengo la kuanzishwa TSC ni kuongeza ufanisi katika kuwahudumia Walimu waliopo kwenye utumishi wa umma wanaofundisha kwenye Shule za Msingi na Sekondari Tanzania Bara.

"Mpaka kufikia Septemba 30, 2022, Tume inahudumia jumla ya Walimu 266,388 Tanzania Bara, wakiwemo 177,956 wa Shule za Msingi na 88,432 wa Shule za Sekondari," alisema

MAFANIKIO YALIYOPATIKANA WAKATI WA SERIKALI YA AWAMU YA SITA

Katibu huyo alieleza kuwa katika kipindi cha kuanzia Machi, 2021 hadi Septemba, 2022, TSC imefanikiwa kutekeleza majukumu mbalimbali ambayo yameendelea kuboresha mazingira ya Walimu na Sekta ya Elimu kwa ujumla.

"Jumla ya Walimu 16,749 waliajiriwa, wakiwemo 8,949 wa Shule za Msingi na 7,800 wa Shule za Sekondari na jumla ya Walimu 15,802 walisajiliwa, Walimu wa Shule za Msingi walikuwa 8,512 na Sekondari walikuwa 7,290. Jumla ya Walimu 6,949 sawa na asilimia 100 walithibitishwa kazini wakiwemo 3,949 wa Shule za Msingi na 3,000 wa Shule za Sekondari," alisema.

Alisema kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa kuhakikisha kila Mwalimu aliyestahili cheo amepandishwa, huku akifafanua kuwa zoezi la kupandisha vyeo walimu ni endelevu na Tume

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akizungumza na vyombo vya habari juu ya mafanikio ya TSC katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita Oktoba, 27, 2022 jijini Dodoma.

TSC YAANIKA MAFANIKIO ILIYOYAPATA KATIKA SERIKALI YA AWAMU YA SITA

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akizungumza na vyombo vya habari juu ya mafanikio ya TSC katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita Oktoba, 27, 2022 jijini Dodoma.

hiyo imekuwa ikishughulikia changamoto ya mwalimu mmoja mmoja kwa wale ambao wamekuwa wakilalamika kucheleweshwa kupandishwa madaraja miaka iliyopita.

"Jumla ya Walimu 47,158 walipandishwa cheo (Walimu 22,943 ni wa Shule za Msingi na 11,524 wa Sekondari kwa mwaka 2021/2022). Aidha kwa mwaka 2020/2021 walimu waliopandishwa cheo ni 126,346. Walimu 12,546 walibadilishiwa vyeo baada ya kujiendeleza kielimu, kati ya hao Walimu 9,059 ni wa Shule za Msingi na Walimu 3,487 ni wa Shule za Sekondari. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya Walimu 3,912 wa Shule za Msingi na Sekondari walistaafu kazi," alisema.

TSC pia imefanikiwa kutafsiri Mkataba wa ajira za Walimu uliokuwa umeandikwa kwa lugha ya kiingereza kwenda katika lugha ya kiswahili ili kuwarahisishia walimu kwenye matumizi ya Mkataba huo.

Katika kuhakikisha kwamba wanazingatia miiko na maadili ya Utumishi wa walimu, Serikali imetoa fedha zilizoiwezesha Tume kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wajumbe wa Kamati za Wilaya zote 139 ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu na Utumishi wa Umma.

Kwa mujibu wa Nkwama Tume hiyo imetoa mwongozo wa kuwajengea uwezo Wakuu wa Shule kusimamia nidhamu ngazi ya Shule. Mwongozo huo ulisambazwa na OR – TAMISEMI, kwa Wakuu wa Shule na unapatikana kwenye tovuti ya Tume - www.tsc.go.tz. Wakuu wa Shule ni Mamlaka ya nidhamu kwa Walimu wanaofanya makosa mepesi kwa mujibu wa Kanuni ya 12(1-3).

Tume hiyo ilifanikiwa

Mkutano wa Katibu wa TSC, Paulina Nkwama na waandishi wa habari ukiwa unaendelea.

TSC YAANIKA MAFANIKIO ILIYOYAPATA KATIKA SERIKALI YA AWAMU YA SITA

kukusanya na kuchambua maoni ya wadau mbalimbali kuhusu marekebisho ya Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu, Sura 448 na hatua nyingine kwa ajili yakufanya marekebisho ya Sheriahiyo zinaendelea.

Akizungumzia masuala ya nidhamu kwa walimu, Nkwama alianza kwa kusema, "Nachukua fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru sana Walimu kwa kazi kubwa ambayo wamekuwa wakiifanya ya kutoa elimu kwa Watoto wetu wa kitanzania, nasisitiza kuwa TSC ni chombo chenu kimeundwa kuwahudumia, hakipo kwa ajili ya kuwafukuza kazi Walimu bali kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa kuwahudumia walimu katika ajira zao na maadili ya utumishi wao."

Alisema kuwa katika kipindi cha mwezi Machi, 2021 hadi Septemba, 2022, Walimu 1,952 walifunguliwa mashauri ya kinidhamu na katika mashauri hayo 1,362 sawa na asilimia 69.8 ya mashauri yote yalihusu utoro, Mashauri 260 sawa na asilimia 13.3 ya mashauri yote yalihusu kughushi vyeti na mashauri 119 sawa na asilimia 6.1 yalihusu mahusiano ya kimapenzi na wanafunzi.

Aliendelea kusema, Mashauri 98 sawa na asilimia 5 yalihusu ukaidi, mashauri 66 sawa na asilimia 3.4 yalihusu ulevi, Mashauri 16 sawa na asilimia 0.8 yalihusu ubadhirifu na mashauri 31 sawa na asilimia 1.6 yalihusu makosa mengineyo.

Katika mashauri 1,642 yaliyoamuliwa; Walimu 919 sawa na asilimia 56 ya adhabu zilizotelewa walifukuzwa kazi, Walimu 234 sawa na asilimia 14.3 hawakupatikana na hatia, Walimu 115 sawa na asilimia 7 ya adhabu zilizotolewa walishushwa cheo, Walimu 89 sawa na asilimia 5.4 walikatwa mshahara asilimia 15 kwa muda wa miaka mitatu na Walimu 143 sawa na asilimia 8.7 walipewa adhabu ya Karipio.

Aliongeza kuwa, walimu 59 sawa na asilimia 3.6 walipewa adhabu ya Onyo na Walimu 77 sawa na asilimia 4.7 walipewa adhabu ya kufidia hasara. Mashauri 310 yapo katika hatua mbalimbali za kuyahitimisha (92 uchunguzi na vikao 218).

Sheria ya TSC inatoa haki kwa Mwalimu kukata rufaa pale ambapo hakubaliani na uamuzi uliotolewa na Mamlaka yake ya nidhamu au Mamlaka yake ya rufaa. Hivyo, Mwalimu asiporidhika na uamuzi wa Mkuu wake wa Shule ambaye ni Mamlaka yake ya kwanza ya nidhamu kwa makosa mepesi ana haki ya kukata rufaa TSC ngazi

Baadhi ya Viongozi wa TSC wakiwa katika Mkutano wa Katibu wa TSC (hayupo pichani) na wanahabari uliofanyika Oktoba 27, 2022 jijini Dodoma.

TSC YAANIKA MAFANIKIO ILIYOYAPATA KATIKA SERIKALI YA AWAMU YA SITA

ya wilaya na kuendelea na ngazi zingine.

"Katika kipindi cha mwezi Machi, 2021 hadi Septemba, 2022; Tume ilitoa uamuzi wa jumla ya rufaa 253 zilizopinga uamuzi uliotolewa na mamlaka ya nidhamu. Katika kipindi hicho, TSC Makao Makuu ilipokea nakala ya rufaa 64 zilizokatwa kwa Rais kupinga uamuzi wa Tume. Tume iliandaa mwenendo na vielelezo vya rufaa 56 na kuwasilisha kwa Rais, Aidha, Tume inaendelea kuandaa mwenendo na uchambuzi wa rufaa 8 zilizobaki kwa hatua ya kuwasilishwa," alifafanua.

"Katika kipindi cha miaka mitatu (2020/2021; 2021/2023; 2022/2023) mfululizo Bajeti ya Tume imeendelea kuongezeka kutoka shilingi Bilioni 14.773, 14.980 na 15.454 sawia. Hii ni kazi kubwa inayofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania," alifafanua.

Kwa mujibu wa Nkwama, ujenzi wa Mfumo wa Tume wa Kielektroniki ujulikanao kwa jina la *Teachers Service Commission Information Management System (TSC-MIS),* ambapo jumla ya Moduli sita (6) zimekamilika, wataalamu wamezifanyia majaribio na mafunzo yamefanyika kwa watumiaji wa majaribio (pilot) ambako Mfumo utaanza kutumika kwa majaribio katika Wilaya 24 nchini ambapo Shilingi 609,840,000.00 zimetumika katika ujenzi wa mfumo huo.

Aliongeza kuwa, ujenzi wa jengo la Tume Makao Makuu chini ya Mkandarasi *SUMA JKT Construction Ltd* lina ghorofa tatu na utagharimu jumla ya Shilingi 6,499,982,353.03 ambapo mpaka sasa Shilingi Milioni 500 zimelipwa kwa Mkandarasi kama malipo ya awali huku Shilingi Milioni 470 zikiwa zimetengwa na kuidhinishwa katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Baadhi ya Viongozi wa TSC wakiwa katika Mkutano wa Katibu wa TSC (hayupo pichani) na wanahabari uliofanyika Oktoba 27, 2022 jijini Dodoma.

VIPAUMBELE VYA TUME KWA MWAKA 2022/ 2023

Kiongozi huyo alisema TSC itasimamia Utumishi na Maendeleo ya Walimu kwa kudumisha Maadili na Nidhamu kwa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari katika Utumishi wa Umma na itahakikisha Walimu wenye sifa ya kupandishwa vyeo na kubadilishiwa kazi wanapata huduma hiyo kwa wakati baada ya kibali kutolewa na Mamlaka husika.

"Tume itaendelea na ujenzi wa jengo la Ofisi za Tume Makao Makuu na kufuatilia ukamilishaji wa Muundo wa Maendeleo ya Utumishi na Mishahara wa Tume pamoja na kuanza kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Masuala ya Utumishi wa Walimu kwa majaribio na kuendelea kutoa elimu kwa watumiaji wa Mfumo huo kuanzia ngazi ya Shule," alisema.

Nkwama alihitimisha kwa kusema kuwa Tume hiyo itaendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa Watumishi wa Tume kwa kuwaongezea ujuzi, kuwapatia ofisi na vitendea kazi na kuongeza uelewa kwa Wadau kuhusu Tume ya Utumishi wa Walimu na majukumu yake.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akisaini kitabu cha wageni wakati alipotembelea Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) mjini Morogoro hivi karibuni. Pembeni ya ni Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Raphael Chibunda.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), Prof. Raphael Chibunda akitoa ufafanuzi wa msuala mbalimbali yanayohusu chuo hicho kwa Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama wakati katibu huyo alipotembelea chuo hicho hivi karibuni.

Kikao kati ya Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama na Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), Prof. Raphael Chibunda kikiwa kinaendelea.

MASHAURI YA NIDHAMU YA WALIMU KILINDI YAPUNGUA

Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kilindi, Mwl. Ayoub Mohamed akifafanua taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo kwa Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami (hayupo pichani) wakati Mkuu huyo wa Kitengo alipotembelea ofisi hiyo hivi karibuni.

Na Mwandishi Wetu – Kilindi.

Hali ya nidhamu kwa walimu wa shule za Msingi na Sekondari wa Wilaya ya Kilindi iliyopo mkoani Tanga imeendelea kuimarika kutokana na juhudi zinazofanywa na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) za kutoa elimu kwa walimu juu ya umuhimu wa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali ya kazi ya utumishi huo.

Kuimarika huko kwa nidhamu kumesaidia kupungua kwa idadi ya mashauri ya walimu kutoka 45 mwaka wa fedha 2019/2020 hadi kufikia mashauri matano (5) kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Hayo yamebainishwa na Afisa wa TSC Wilayani hapo, Mwl. Ayoub Idd Mohamed aliyekuwa akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo kwa niaba ya Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Kilindi wakati Watumishi wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu walipofika ofisini hapo hivi karibuni.

"Mwaka wa fedha 2019/2020 tulikuwa na mashauri 45 mwaka 2020/2021 yalikuwa 28 na mwaka 2021/2022 yalikuwa matano (5).

Tumekuwa tukiwakumbusha walimu nguzo za maadili ya kazi ya ualimu kupitia ziara shuleni na vikao mbalimbali vya pamoja na walimu na haya ndiyo matunda yake," alisema Mwl. Mohamed.

Alieleza kuwa makosa mengi yanayofanywa na walimu ni ya utoro kazini huku akiweka bayana kuwa katika adhabu zilizotolewa katika kipindi cha mwaka 2019/2020 hadi mwezi septemba 2022 jumla ya walimu 60 walifukuzwa kazi, walimu 12 walipewa adhabu nyingine zikiwemo kushushwa cheo, kushushwa mshahara nk na walimu tisa (9) waliachiwa huru baada ya tuhuma zao kutothibitika.

Mohamed aliongeza kuwa

Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kilindi, Mwl. Ayoub Mohamed (kushoto) akifafanua taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo kwa Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami wakati Mkuu huyo wa Kitengo alipotembelea ofisi hiyo hivi karibuni.

MASHAURI YA NIDHAMU YA WALIMU KILINDI YAPUNGUA

sababu nyingine ya kuimarika kwa nidhamu ya Walimu katika wilaya hiyo ni kunatokana na Wakuu wa Shule kuwa na uelewa na kutekeleza majukumu yao ya mamlaka ya nidhamu kwa walimu ikiwa ni pamoja na kutoa elimu na kuchukua hatua stahiki kwa makosa madogo madogo kitu ambacho kimesaidia walimu kuzingatia miiko na maadili ya kazi yao.

"Wakuu wa shule kama mamlaka ya nidhamu kwa walimu walioko chini yao wanatekeleza majukumu yao katika kuwasimamia walimu na hii imesaidia walimu kusaidiwa mapema kabla ya makosa kuwa makubwa kitu kinachoweza kusababisha hata kufukuzwa kazi pale tuhuma zinapothibitika," aliongeza.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami akiongea na Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kilindi, Mwl. Ayoub Mohamed wakati Mkuu huyo wa Kitengo alipotembelea ofisi hiyo hivi karibuni.

Akizungumzia kuhusu maendeleo ya walimu, Mwl. Mohamed alisema mwezi Juni 2022, Wilaya ya Kilindi kupitia ofisi ya TSC ilipandisha vyeo walimu 89 baada ya kupokea kibali toka kwa Katibu Katibu Mkuu Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na kwa kuzingatia kama iliyowasilishwa Tume hiyo ikiwabadilishia vyeo walimu watano (5).

Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kilindi, Mwl. Ayoub Mohamed akimkabidhi taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami wakati Mkuu huyo wa Kitengo alipotembelea ofisi hiyo hivi karibuni.

"Tume iliwapandisha walimu vyeo na kuwabadilishia cheo kwa mujibu wa maelekezo yote yaliyoelekezwa na Katibu Mkuu Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Walimu wote waliopandishwa vyeo wanapata mishahara mipya na wote waliandikiwa barua na kukabidhiwa," alisema.

Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kilindi inahudumia shule za msingi 111, shule shikizi 41 na shule za sekondari 22 za Serikali huku ikihudumia Jumla ya walimu 1315 wakiwemo walimu wa 958 wa shule za Msingi na walimu 357 wa shule za Sekondari.

TSC YAPONGEZWA KWA KUTEKELEZA MAJUKUMU YAKE KWA WELEDI

Na Mwandishi Wetu – Dodoma.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Festo Dugange ameipongeza Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo inayotolewa na Serikali.

Naibu Waziri huyo ametoa kauli hiyo wakati akifungua Mkutano Baraza la Wafanyakazi wa Tume ya Utumishi wa Walimu uliofanyika Oktoba 18, 2022 katika Ukumbi wa Jengo la Takwimu jijini Dodoma.

"Nawashukuru Menejimenti na watumishi wa Tume kwa namna mnavyojitoa katika kutekeleza majukumu ya Tume na hivyo kufanya kazi ya viongozi wanaowasimamia kuwa nyepesi" amesema.

Aidha, ameipongeza Serikali ya awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan, kwa kuwapandisha vyeo kwa mkupuo zaidi ya Walimu 160,888 na kuwabadilishia vyeo walimu 1,581 kwa miaka miwili mfululizo 2020/21 na 2021/22.

"Walimu kama watumishi wengine wa umma wameendelea kunufaika na malipo ya malimbikizo ya madai mbalimbali ya mishahara na yasiyo ya mishahara, ajira za watumishi walimu 14,949 (2020/21) na 9,800 (2021/22), kupunguza kodi kutoka asilia 9 hadi 8, kuondoa

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba akitoa neno la kumkaribisha Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Dkt. Festo John Dugange (Mb) kwa ajili ya kufungua Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi, Oktoba 18, 2022 jijini Dodoma.

Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ambaye pia ni Katibu wa Tume hiyo, Mwl. Paulina Nkwama akitoa hotuba wakati wa ufunguzi wa Mkutano Baraza la Wafanyakazi la TSC Oktoba 18, 2022 jijini Dodoma.

TSC YAPONGEZWA KWA KUTEKELEZA MAJUKUMU YAKE KWA WELEDI

Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Dkt. Festo John Dugange (Mb) (katikati), Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba (kushoto) na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la TSC ambaye pia ni Katibu wa Tume hiyo, Mwl. Paulina Nkwama wakiimba wimbo wa mshikamano daima wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Baraza hilo uliofanyika Oktoba, 18, 2022 jijini Dodoma.

tozo ya thamani ya elimu ya juu na wategemezi wa Bima kutoka umri wa miaka 18 hadi 21" ameongeza.

Katika hatua nyingine, ameipongeza Tume hiyo kwa kutowafumbia macho walimu wasiozingatia maadili ya kazi yao.

"Jumla ya walimu 11,396 wamechukuliwa hatua za kinidhamu kutokana na makosa mbalimbali yaliyofanywa na walimu. Nimeona kuwa, kosa la utoro limeongoza kwa kuwa na walimu 7,579 (66.5%), na asilimia zilizobaki ni makosa mengine. Nitoe rai kwa Tume kuendelea kuwaelimisha Walimu kutambua wajibu wao ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa weledi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu" amesema.

Kwa upande wake, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama amesema masuala yaliyojadiliwa katika mkutano huo ni pamoja na Kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Tume kwa kipindi cha Mwaka 2021/22 na mwelekeo wa Bajeti iliyopitishwa kwa mwaka wa fedha 2022/23.

"Lakini pia kupitisha Katiba ya mfuko wa Kufarijiana, Katiba ya SACCOS ya Tume ya Utumishi wa Walimu; Kuwajulisha Wajumbe wa Baraza kuhusu wajibu na haki katika kutekeleza majukumu ya Baraza" amesema.

Pamoja na hayo, amesema mbali na ufinyu wa Bajeti, katika kipindi cha miaka sita (6) tangu Tume ilipoanza kutekeleza majukumu yake mwezi Julai, 2016 hadi kufikia mwezi Juni, 2022 Tume kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI pamoja na wadau wake imefanikiwa kutekeleza mambo mbalimbali ikiwemo kufanya tathmini ya hali ya walimu nchini.

"Zoezi hili lililofanywa na Tume kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa kutumia Mfumo wa TAMISEMI ujulikanao kama *School Information System (SIS).* Zoezi hilo lilibaini kuwa, mahitaji ya walimu kwa Shule za Msingi ni 298,313, waliopo ni 173,591."

"Aidha, mahitaji ya walimu Shule za Sekondari ni 175,592, waliopo ni 84,700. Taarifa hiyo iliwasilishwa kwa Katibu Mkuu OR – TAMISEMI na kuwezesha walimu 9,800 kuajiriwa mwezi Juni, 2022" ameogeza.

Malengo ya kuanzishwa kwa Tume ya Utumishi wa Walimu ni kuongeza ufanisi katika kuwahudumia Walimu ambao ni kundi kubwa lenye zaidi ya asilimia hamsini (50%) ya watumishi wote wa Umma.

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba (kushoto) na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la TSC ambaye pia ni Katibu wa Tume hiyo, Mwl. Paulina Nkwama (katikati) pamoja na Katibu wa Baraza hilo, Laurence Chankan (kulia) wakiwa katika mkutano wa Baraza hilo uliofanyika Oktoba, 18, 2022 jijini Dodoma.

Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Zachary Dida akitoa ufafanuzi wakati wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi la TSC uliofanyika Oktoba 18, 2022 jijini Dodoma.

Baadhi wa Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakiwa katika Mkutano wa Baraza hilo uliofanyika Oktoba 18, 2022 jijini Dodoma.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Dkt. Festo John Dugange (Mb) (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wajumbe wa menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC). Wengine (waliokaa) ni Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (wa pili kutoka kushoto), Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kulia), Naibu Katibu Mkuu wa TUGHE Taifa, Rugemalira Rutatina (wa kwanza kutoka kushoto) na Katibu wa Baraza la Wafanyakazi la TSC, Laurence Chankan (wa kwanza kutoka kulia).

Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Dkt. Festo John Dugange (Mb) (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na wajumbe wa Baraza la wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC). Wengine (waliokaa) ni Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (wa pili kutoka kushoto), Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kulia), Naibu Katibu Mkuu wa TUGHE Taifa, Rugemalira Rutatina (wa kwanza kutoka kushoto) na Katibu wa Baraza la Wafanyakazi la TSC, Laurence Chankan (wa kwanza kutoka kulia).

Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Dkt. Festo John Dugange (Mb) (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na wajumbe wa Baraza la wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC). Wengine (waliokaa) ni Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (wa pili kutoka kushoto), Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kulia), Naibu Katibu Mkuu wa TUGHE Taifa, Rugemalira Rutatina (wa kwanza kutoka kushoto) na Katibu wa Baraza la Wafanyakazi la TSC, Laurence Chankan (wa kwanza kutoka kulia).

Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Dkt. Festo John Dugange (Mb) (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na wajumbe wa Baraza la wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC). Wengine (waliokaa) ni Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (wa pili kutoka kushoto), Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kulia), Naibu Katibu Mkuu wa TUGHE Taifa, Rugemalira Rutatina (wa kwanza kutoka kushoto) na Katibu wa Baraza la Wafanyakazi la TSC, Laurence Chankan (wa kwanza kutoka kulia).

Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Dkt. Festo John Dugange (Mb) (mbele mwenye tai) akiingia kwenye Ukumbi uliopo kwenye Jengo la Takwimu jijini Dodoma kwa ajili ya kufungua Mkutano wa Barazala Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) lililofanyika Oktoba 18, 2022.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Dkt. Festo John Dugange (Mb) (kushoto) akisalimiana na Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi la TSC lililofanyika Oktoba 18, 2022 jijini Dodoma. Katikati ni Katibu wa TSC Paulina Nkwama.

TSC BUSEGA YATOA MAFUNZO KWA WALIMU WAPYA KAZINI

Na Mwandishi Wetu – Busega.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Busega imetoa mafunzo kwa walimu walioajiriwa hivi karibuni kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kuelewa taratibu mbalimbali za Utumishi wa Walimu.

Mafunzo hayo yalitolewa tarehe 20/10/2022 wilayani hapo ambapo mada zilizotawala zilikuwa ni pamoja na Maadili na Nidhamu ya kazi ya Ualimu, Ajira na Maendeleo ya Walimu, Nguzo za Maadili ya kazi ya Ualimu pamoja na Elimu ya fedha na Mikopo yenye riba nafuu.

Watoa mada katika mafunzo hayo walitoka wilayani hapo ambao walikuwa ni Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Busega, Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Afisa Utumishi, Afisa Elimu Sekondari, Afisa Elimu Msingi, Katibu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) Wilaya, Meneja wa Benki ya NMB na Meneja wa Benki ya CRDB.

Mafunzo ya Walimu wa Ajira mpya wilayani Busega yakiwa yanaendelea.

WALIMU 11,022 WAPATIKANA NA MAKOSA MBALIMBALI KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MITANO (2016/17 – 2021/22).

- Utoro kazini ukiongoza kwa asilimia 68.8;
- Kughushi vyeti ikishika namba mbili (13%), namba tatu ni Ukiukaji wa Maadili ya Kazi ya Ualimu (11.7%); na
- Mahusiano ya kimapenzi na wanafunzi yakiwa ni asilimia tatu na ulevi asilimia moja.

Na Mwandishi Wetu – Dodoma.

Katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2016/17 hadi 2021/22 jumla ya walimu 11,022 walipatikana na makosa mbalimbali ya kinidhamu yakiwemo; utoro kazini, kughushi vyeti vya kitaaluma, mahusiano ya kimapenzi na wanafunzi, ukaidi, ulevi wakati wa saa za kazi, ukiukaji wa maadili na miiko ya kazi ya ualimu.

Takwimu hizo zimetolewa katika Taarifa ya Mapitio ya Maadili na Miiko ya Kazi ya Ualimu iliyoandaliwa na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ikiwa ni wasilisho kwa wadau wa maendeleo juu ya dhana ya maadili na miiko ya kazi ya ualimu iliyowasilishwa hivi karibuni.

Taarifa hiyo imesema mantiki ya kufanya mapitio hayo imetokana na kuwepo kwa ongezeko la ukiukwaji wa maadili ya ualimu unaofanywa na walimu hadi kufikia hatua ya kuidhalilisha taaluma hiyo.

Taarifa hiyo imesema kuwa baadhi ya walimu wamekuwa wakijihusisha na vitendo vya ukatili na udhalilishaji kwa wanafunzi waliopewa dhamana ya kuwalea na hivyo kusababisha kuwepo kwa matokeo hasi kwa wanafunzi wanaowafundisha kwa kuiga kutoka kwa walimu wao na kujihusisha katika mienendo isiyofaa na hatimaye kutofanya vizuri kwenye masomo yao na kuwa na maadili yasiyofaa kwa jamii.

Aidha, taarifa hiyo imesema kuwa TSC imepewa jukumu la kusimamia maadili ya walimu chini ya kifungu cha 5 (C) cha Sheria Sura Na.448 na katika kutekeleza jukumu hilo TSC kupitia Ofisi zake za Wilaya zote 139 hapa nchini imekua ikitoa elimu ya maadili na nidhamu kwa walimu na kuchukua hatua za kinidhamu kwa walimu wanaokiuka maadili au miiko ya kazi ya ualimu.

Taarifa hiyo imeongeza kuwa, Miiko na Maadili ya Kazi ya Ualimu ilianzishwa kwa lengo la kuwafanya walimu kuwa waadilifu katika utendaji kazi wao kwa kuzingatia maadili na miiko ya kazi yao, kudumisha imani ya walimu kwa Umma na kuwafanya walimu wajue kuna mambo ambayo hawapaswi kuyafanya kwa mujibu wa taaluma yao.

Pamoja na hilo taarifa hiyo imesema ni dhahiri elimu imejikita katika maadili kwani bila maadili hakuna elimu iliyo bora; "Walimu kama ilivyo kada nyingine mfano; Madaktari, Wauguzi, Wahandisi, Wanasheria, na wengineo wanayo maadili na miiko inayoongoza taaluma zao ambapo pamoja na hayo yapo Maadili ya Utumishi wa Umma ambayo hayana budi kuzingatiwa na Watumishi wote wa Umma wakiwemo Walimu."

Ikizitaja sehemu ya changamoto zilizopo za Kanuni na Miiko ya Maadili ya Walimu katika mapitio hayo ambazo zimesababisha ongezeko la mmomonyoko wa maadili kwa walimu na wanafunzi na kuathiri suala zima la elimu na maadili nchini kuwa ni pamoja na Maadili na Miiko iliyopo kueleza wajibu wa Mwalimu kwa mtoto, kwa kazi yake, kwa mwajiri, kwa jamii na Taifa.

Taarifa hiyo imesema lengo kuu la mapitio hayo ni kuhakikisha taaluma ya Ualimu inakuwa na Walimu waadilifu na wenye kuwajibika huku malengo mahsusi yakiwa ni pamoja na kuwawezesha walimu kufanya kazi kwa bidii na uadilifu kwa kuzingatia miiko ya kitaaluma ya kazi yao, kuwawezesha walimu kutambua mambo ambayo walimu hawapaswi kuyafanya kwa mujibu wa taaluma yao, kuwawezesha walimu kutambua hatua zitakazochukuliwa endapo hatazingatia maadili na miiko ya taaluma ya ualimu iliyowekwa, kuwafanya wanafunzi kujifunza tabia njema kutoka kwa walimu wao kwa kuongeza utii, uaminifu, bidii kwenye masomo na kuwa na tabia njema kwa jamii na Taifa kwa ujumla, kuwawezesha wasimamizi wa walimu kufanya maamuzi sahihi kwa kuzingatia Kanuni za Maadili na Miiko ya kazi ya ualimu, kuwawezesha walimu kutambua na kuzingatia haki za mtoto wanayemlea kimwili, kiakili na kiroho.

Miiko na Maadili ya Kazi ya Ualimu katika Utumishi wa Walimu yalianzishwa na chombo kilichoundwa kwa ajili ya kuhudumia Walimu kilichojulikana kama Unified Teachers' Service (U.T.S) ambacho kilianzishwa kwa Sheria ya U.T.S Na. 6 (1) ya mwaka 1962 ambapo Waziri wa Elimu kwa wakati huo ambaye chombo hiki kilikuwa chini yake alipewa dhamana kwa mujibu wa Sheria hiyo kutengeneza Kanuni na Miiko ya Kazi ya Ualimu. Hivi sasa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imepewa jukumu la kusimamia Maadili na Nidhamu za Walimu waliopo kwenye Utumishi wa Umma Tanzania Bara kwa mujibu wa Sheria ya TSC Namba 25 ya mwaka 2015, chini ya Kifungu cha 5 (c) (j).

TSC YATOA MAFUNZO UTUMIAJI WA MFUMO WA *TSCMIS*

Na Mwandishi Wetu – Morogoro.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeendesha mafunzo ya uelewa wa ufanyaji kazi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Tume (TSCMIS) ikiwa ni mwanzo wa matumizi ya mfumo huo unaolenga kurahisisha utoaji wa huduma katika masuala ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu nchini.

Akifungua Mafunzo hayo yaliyofanyika Oktoba 10 - 13, 2022 katika Ukumbi wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine kampasi ya Mazimbu – Morogoro, Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama alisema kuwa mfumo wa *TSCMIS* utarahisisha na kuboresha utendaji kazi wa shughuli za kila siku katika kuwahudumia walimu kwenye masuala ya ajira (usajili na kuthibitishwa kazini), maendeleo ya Walimu (kupandishwa vyeo na kubadilishiwa muundo wa utumishi), mafao, mashauri ya nidhamu pamoja na rufaa za walimu.

"Matumizi ya mfumo yataongeza ufanisi katika kushughulikia Utumishi wa Walimu na utamfanya mwalimu asihangaike kutafuta huduma. Kama atakuwa na hoja zake ataingia kwenye mfumo atatoa taarifa ataweka na hoja yake atatuma. Akishatuma ana uwezo wa kufuatilia na kuona hoja yake ilipofikia na pale itakapokuwa imejibiwa atapata majibu hapo hapo. Hivyo, kwa kupitia simu ya mkononi mwalimu atapata huduma zote za kiutumishi," alisema Nkwama.

Aliongeza kuwa mfumo huo utasaidia kuondoa changamoto za upatikanaji wa taarifa kwa wakati hususan taarifa za wilaya ambazo mara kwa mara zinachelewa kuwasilishwa TSC Makao Makuu kwa kuwa mfumo huo una uwezo wa kutunza na kutoa taarifa ya kila kinachofanyika kuanzia ngazi ya shule hadi TSC Makao Makuu.

Aidha, Katibu huyo aliongeza kuwa miongoni mwa majukumu ya TSC ni kushughulikia mashauri ya nidhamu ya walimu kwa haki

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu TSC, Mwl. Paulina Nkwama akitoa hotuba ya ufunguzi wa mafunzo ya uelewa wa ufanyaji kazi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Tume (TSCMIS) yanayofanyika Oktoba 10 -13, 2022 katika Ukumbi wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine kampasi ya Mazimbu – Morogoro.

Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu wa TSC, Zachary Dida akitoa neno la kumkaribisha Katibu wa TSC wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya uelewa wa ufanyaji kazi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Tume (TSCMIS) uliofanyika Oktoba 10, 2022 katika Ukumbi wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine kampasi ya Mazimbu – Morogoro.

TSC YATOA MAFUNZO UTUMIAJI WA MFUMO WA *TSCMIS*

Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA wa TSC ambaye pia ni Mratibu na Msimamizi wa ujenzi wa mfumo huo, Bi. Kainda Ndasa kitoa taarifa ya ujenzi wa mfumo wa kilelektoniki wa TSC (TSCMIS) wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi wa TSC juu ya utumiaji wa mfumo huo.

na kueleza kuwa kutumika kwa mfumo huo kutasaidia Tume hiyo kutasaidia kuondoa changaoto mbalimbali katika kuendesha mashauri kwenye ngazi ya shule na ngazi ya wilaya.

"Katika uendeshaji wa mashauri ya nidhamu kumekuwa na changamoto ndogondogo ambazo wakati mwingine zimesababisha mashauri ya walimu kuchelewa kumalizika. Pale unapokuta shauri limeendeshwa lakini taratibu zimekiukwa, mwalimu anapokata rufaa shauri hilo linarudishwa lianze upya. Lakini kupitia mfumo huu tutakuwa na uwezo wa kuona shauri tangu linapofunguliwa, hivyo kama tutaona kuna sehemu haiko sawa ni rahisi kutoa ushauri stahiki mapema," alisema.

Nkwama alisisitiza kuwa mara baada ya mafunzo hayo anataka mfumo huo uanze kutumika huku akiweka bayana kuwa hatakubali kuona wilaya ambazo zimepata mafunzo zinaleta visingizio vya kutotumia mfumo huo na kuwataka washiriki hao kuwa mfano mzuri katika matumizi ya mfumo huo.

"Sasa ninyi mmekuwa mabalozi, ninatarajia kuwa baada ya kutoka hapa mtakwenda kuutumia mfumo huu kama inavyotakiwa. Tukumbuke wakuu

Mshiriki wa mafunzo ya uelewa wa ufanyaji kazi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Tume (TSCMIS) ambaye pia ni Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Ilala, Subira Mwakibete akitoa neneo la shukrani kwa Katibu wa TSC (hayupo pichani) wakati wa ufunguzi wa mafanzo hayo uliofanyika Oktoba 10, 2022 katika Ukumbi wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine kampasi ya Mazimbu – Morogoro.

Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Morogoro, Lusubilo Mwaisunga akiwakarisha Wilaya ya Morogoro washiriki wa mafunzo ya utumiaji wa mfumo wa TSCMIS yanayofanyika kwa siku nne wilayani Morogoro.

TSC YATOA MAFUNZO UTUMIAJI WA MFUMO WA *TSCMIS*

Mmoja wa wakufunzi wa Mfumo wa Kielektroniki wa TSC (TSCMIS) akitoa wasilisho juu matumizi ya mfumo huo.

wa shule wanasajili wanafunzi kwa ajili ya kufanya mitihani ya Taifa kwa mfumo. Sasa itakuwa ni jambo lisiloeleweka kwa wewe mtumishi wa TSC kuanza kuleta visingizio ili tu usitumie mfumo, kwa kweli hatutaelewana," alisema Nkwama.

Nkwama pia alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa jitihada zake za kuwajali walimu na kuamua kuitengea TSC bajeti kwa ajili ya ujenzi na uendeshaji wa mfumo huo. Vilevile, alitumia fursa hiyo kumpongeza Mhe. Angellah Kairuki kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambapo alieleza kuwa Waziri huyo ameelekeza kuongeza kasi ya matumizi ya mifumo ya kielektoniki katika shughuli za Serikali ili kuboresha upatikanaji wa huduma kwa wananchi.

Awali akitoa taarifa za maendeleo ya mfumo huo, Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA wa TSC ambaye pia ni Mratibu na Msimamizi wa ujenzi wa mfumo

Washiriki wa mafunzo ya utumiaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSCMIS) wakiwa katika mafunzo hayo ndani ya Ukumbi wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine kampasi ya Mazimbu – Morogoro, Oktoba 10, 2022.

TSC YATOA MAFUNZO UTUMIAJI WA MFUMO WA *TSCMIS*

huo, Bi. Kainda Ndassa, alisema kuwa ujenzi wa mfumo huo uliochukua muda wa miaka miwili ulikamilika tarehe 31/08/2022 ambapo kwa nyakati tofauti ulihusisha wataalam kutoka Taasisi mbalimbali ikiwewo Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi ya Rais Menejeimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mamlaka ya Serikali Mtandao na Vyuo Vikuu vya Sokoine na Mzumbe.

"Ninawashukuru Maafisa Wataalamu wote wa TEHAMA kutoka Taasisi mbalimbali za Serikali zikiwemo Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA), na Chuo Kikuu Mzumbe) kwa kuratibu zoezi zima la uundaji wa mfumo huu," alisema.

Alisema kuwa ujenzi wa Mfumo wa TSCMIS ambao unajumuisha moduli sita (6) umezingatia Mwongozo uliotolewa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) na kufuata hatua mbalimbali katika ujenzi wake ambazo ni pamoja na kubainisha mahitaji *(Requirement gathering)*, kusanifu na kujenga Mfumo *(System Design and Development)*, majaribio (*Testing*), kusimika na kusimamia Mfumo *(Operational and Maintenance)*.

Alizitaja moduli hizo kuwa ni *'Disciplinary, Appeal, Gratuity and Pension Computation, Complaints, Registration, Visitors and Helpdesk'* ambazo zinahusika na uendeshaji wa mashauri ya nidhamu na rufaa, ukokotoaji wa mafao ya ajira za mkataba, malalamiko na dawati la msaada kwa wateja.

Mafunzo hayo yaliwahusisha watumishi wa TSC kutoka Wilaya za Mikoa ya Mwanza, Iringa, Dodoma, Dar es Salaam na Wilaya ya Morogoro ambaye ni mwenyeji wa mafunzo hayo huku Wilaya ya Kishapu ikishiriki kama Wilaya ya mfano. Vilevile baadhi ya Wakuu wa Shule kutoka Shule za Msingi na Sekondari walishiriki.

Washiriki wa mafunzo ya utumiaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSCMIS) wakiwa katika mafunzo hayo ndani ya Ukumbi wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine kampasi ya Mazimbu – Morogoro, Oktoba 10, 2022.

Washiriki wa mafunzo ya utumiaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSCMIS) wakifuatilia mafunzo hayo ndani ya Ukumbi wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine kampasi ya Mazimbu – Morogoro, Oktoba 10, 2022.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wajumbe wa Menejimenti ya Tume pamoja na Maafisa wa TSC kutoka Wilaya za Mkoa wa Iringa wakati wa mafunzo ya utumiaji wa Mfumo wa TSCMIS yaliyofanyika Oktoba 10 – 13 mjini Morogoro.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wajumbe wa Menejimenti ya Tume pamoja na Maafisa wa TSC kutoka Wilaya ya Kishapu na Morogoro wakati wa mafunzo ya utumiaji wa Mfumo wa TSCMIS yaliyofanyika Oktoba 10 – 13 mjini Morogoro.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wajumbe wa Menejimenti ya Tume pamoja na baadhi ya Wakuu wa Shule walioshiriki mafunzo ya utumiaji wa Mfumo wa TSCMIS yaliyofanyika Oktoba 10 – 13 mjini Morogoro.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wajumbe wa Menejimenti ya Tume pamoja na maafisa kutoka TSC Makao Makuu na wakufunzi mafunzo ya utumiaji wa Mfumo wa TSCMIS yaliyofanyika Oktoba 10 – 13 mjini Morogoro.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wajumbe wa Menejimenti ya Tume pamoja na Maafisa wa TSC kutoka Wilaya za Mkoa wa Mwanza wakati wa mafunzo ya utumiaji wa Mfumo wa TSCMIS yaliyofanyika Oktoba 10 – 13 mjini Morogoro.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wajumbe wa Menejimenti ya Tume pamoja na Maafisa wa TSC kutoka Wilaya za Mkoa wa Dar es Salaam wakati wa mafunzo ya utumiaji wa Mfumo wa TSCMIS yaliyofanyika Oktoba 10 – 13 mjini Morogoro.

BILIONI 8.9 KUTUMIKA KATIKA MIRADI YA KUBORESHA MIUNDOMBINU YA ELIMU NCHINI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2022- 2023.

- Nyumba za Walimu 52, Madarasa 99, Matundu 792 ya Vyoo, Maabara 10 za Masomo ya Sayansi na Mabweni 10 kujengwa;
- Miundombinu ya wanafunzi wenye mahitaji maalum yajumuishwa; na
- Vigezo vya unufaika ni pamoja na shule zenye uhaba mkubwa wa miundombinu kulingana na idadi ya wanafunzi, usajili wa shule na maombi ya ufadhili.

Na. Mwandishi Wetu - Dar Es Salaam.

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) imepanga kutumia kiasi cha Sh. Bilioni 8.9 kwa ajili ya kufadhili miradi ya kuboresha miundombinu ya elimu nchini kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu yake ya kusaidia jitihada za Serikali katika kuwezesha upatikanaji wa elimu bora kwa usawa nchini.

Hayo yalibainishwa na Mtendaji Mkuu wa TEA, Bi. Bahati Geuzye wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji na uelekeo wa Bajeti ya TEA katika ukumbi wa mikutano wa Idara ya Habari - MAELEZO jijini Dar es Salaam tarehe Agosti 4, 2022.

Alifafanua kuwa kiasi hicho cha fedha kitatumika kujenga jumla ya miradi 96 katika Shule za Msingi na Sekondari Tanzania bara pamoja na Taasisi mbili za elimu ya juu Tanzania Zanzibar.

Alisema miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa madarasa 99, matundu ya vyoo 792, maabara 10 za masomo ya sayansi kwa ajili ya shule tano za sekondari, nyumba za Walimu 52 na mabweni 10.

Miradi mingine ni ujenzi wa miundombinu ya wanafunzi wenye mahitaji maalum inayojumuisha madarasa 10, matundu ya vyoo 40 pamoja na mabweni mawili katika shule sita zenye watoto wenye mahitaji maalum.

Aliongeza kuwa vigezo vinavyotumika kuchagua wanufaika wa ufadhili wa Mfuko wa Elimu ni pamoja na kuangalia shule zenye uhaba mkubwa wa miundombinu kutokana na kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi, usajili wa shule na orodha ya maombi ya ufadhili iliyoko kwenye kanzidata za TEA.

Bi. Geuzye alisema katika mwaka wa fedha 2021/2022, kiasi cha Shs. Bilioni 8.8 zilitumika kugharimia ufadhili wa miradi 160 ya kuboresha miundombinu ya elimu katika shule 151 nchini ikijumuisha ujenzi wa madarasa 210 katika Shule 70, Maabara 2 za sayansi katika shule za sekondari zenye mahitaji maalum, Matundu ya vyoo 1,920 katika shule 80, vifaa vya kujifunzia na kufundishia na uendelezaji wa miundombinu katika shule tisa za watoto wenye mahitaji maalum pamoja na ofisi mbili za Walimu katika shule mbili.

Mtendaji Mkuu wa TEA aliendelea kuhimiza wadau mbalimbali wa elimu kutoa ufadhili wa miradi ya elimu kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa ambao una jukumu la Kisheria la kuratibu michango inayotolewa katika Sekta ya Elimu nchini ili kuwezesha Serikali kuwa na takwimu sahihi za wachangiaji na thamani ya michango.

"Taasisi au watu wanaochangia kupitia TEA wanatambuliwa rasmi kwa kupewa cheti maalum na wanaweza kuomba nafuu ya kodi kwa Kamishna wa Kodi ya Mapato Nchini (TRA). Hii ni kwa mujibu wa Kifungu cha 12 cha Sheria ya Mfuko wa Elimu ya Mwaka 2001 na Kifungu cha 16 cha Sheria ya Mapato ya mwaka 2006." Alisema Mtendaji Mkuu huyo

Kuhusu utekelezaji wa Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi (SDF), Mtendaji Mkuu huyo wa TEA alisema hadi kufikia mwezi Juni 2022 kiasi cha Shs Bilioni 8.6 kimetolewa kwa ajili ya kufadhili miradi 81 ambapo jumla ya wanufaika 33,510 ikiwa ni Wanaume 17,257 (51.5%) na Wanawake 16,253 (48.5%) wamepatiwa mafunzo.

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) ni Taasisi ya Umma inayofanya kazi chini ya usimamizi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. TEA inaratibu Mfuko wa Elimu wa Taifa ambao unasaidia jitihada za Serikali katika kuboresha miundombinu ya elimu kwa lengo la kuongeza ubora wa elimu na upatikanaji wake kwa usawa. Aidha, TEA inaratibu Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi (SDF) unaofadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Benki ya Dunia.

NKWAMA APONGEZWA KWA KUIMARISHA UHUSIANO KATI YA TSC NA OFISI YA ELIMU MKOA, HALMASHAURI

Na Mwandishi Wetu – Morogoro.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama amepongezwa kwa kuimarisha uhusinao na ushirikiano kati ya Tume hiyo na ofisi za Elimu za Mikoa na Halmashauri nchini.

Pongezi hizo zimetolewa Oktoba 10, 2022 na Katibu Tawala Msaidizi (Elimu) Mkoa wa Morogoro, Germana Mng'aho wakati Katibu wa TSC alipotembelea Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro ambapo TSC ilikuwa inaendesha mafunzo ya utumiaji wa mfumo wa Kielektoniki (TSCMIS) kwa watumishi wake mkoani humo.

"Nakupongeza Katibu kwa utendaji kazi wako mzuri, tangu umeingia katika nafasi hiyo tumeona mabadiliko makubwa. Kumekuwa na ushirikiano mkubwa kati ya TSC na sisi Maafisa Elimu katika ngazi ya Halmashauri kitu ambacho hakikuwepo siku za nyuma," alisema.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akisaini daftari la wageni kwenye Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro Oktoba 10, 2022. Pembeni yake ni Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali TSC, Gerard Chami.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (wa kwanza kushoto) akiongea na Katibu Tawala Msaidizi (Elimu) Mkoa wa Morogoro, Bi. Germana Mng'aho wakati alipotembelea Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro Oktoba 10, 2022.

Afisa Elimu huyo aliongeza kuwa ushirikiano huo umesaidia vyombo hivyo vya elimu kutatua changamoto za walimu kwa pamoja na kwa wakati, hivyo kusaidia walimu kupata huduma bora ikiwa ni sehemu ya kutimiza azma ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kuboresha mazingira ya utendaji kazi ya walimu.

Aidha, aliipongeza TSC kwa kuamua kujenga mfumo wa TSCMIS kwa ajili ya kutoa majibu ya changamoto mbalimbali

NKWAMA APONGEZWA KWA KUIMARISHA UHUSIANO KATI YA TSC NA OFISI YA ELIMU MKOA, HALMASHAURI

zinazowakabili walimu huku akieleza kuwa mfumo huo utawafanya walimu wasilazimike kuondoka kwenye vituo vyao vya kazi kwa ajili ya kutafuta huduma.

Kwa upande wake Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama alisema kuwa mfumo wa TSCMIS unatarajiwa kuanza kutumika kwa Wilaya za Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Mwanza na Wilaya za Kishapu na Morogoro ambapo mafunzo yametolewa huku akieleza kuwa dhamira ya TSC ni kuona ofisi zake zote zinatumia mfumo huo kurahisisha kuhudumia walimu kwa wakati, weledi na uwazi.

Katibu Tawala Msaidizi (Elimu) Mkoa wa Morogoro, Bi. Germana Mng'aho akiongea na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (hayupo pichani) katika Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro Oktoba 10, 2022.

Alieleza kuwa mfumo huo una faida lukuki kwa TSC na wadau ikiwa ni pamoja na kuboresha utekelezaji wa majukumu katika kuwahudumia walimu kwa ufanisi na kuondoa malalamiko ya walimu yanayosababishwa na kuchelewa kupata huduma.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kulia) akiongea Katibu Tawala Msaidizi (Elimu) Mkoa wa Morogoro, Bi. Germana Mng'aho wakati alipotembelea Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro Oktoba 10, 2022.

"Mfumo wa TSCMIS utarahisisha mchakato wa kushughulikia mashauri ya nidhamu na Rufaa za Walimu kuanzia ngazi ya Shule, Ofisi za Wilaya hadi Makao Makuu. Vilevile, Mfumo utasaidia kusimamia na kufanya ufuatiliaji wa hatua za Mashauri ya Nidhamu na Rufaa za Walimu kuanzia ngazi ya Shule hadi Makao Makuu," alisema.

Aliongeza kuwa mfumo huo utakuwa na uwezo wa kutoa mrejesho (*feedback*) kuhusu malalamiko yaliyowasilishwa pamoja na kupunguza matumizi ya karatasi na kuboresha utunzaji na upatikanaji wa taarifa pamoja na kurahishisha mawasiliano na utendaji kazi katika Ofisi za Tume kuanzia ngazi ya Wilaya, Makao Makuu na Wadau mbalimbali.

WALIMU 87 MSINGI, 17 SEKONDARI WAHITAJIKA KUMALIZA TATIZO LA UPUNGU WA WALIMU PANGANI

Na Mwandishi Wetu - Pangani.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Pangani imesema wilaya hiyo inahitaji Walimu 87 wa shule za Msingi na Walimu 17 wa Sayansi kwa upande wa shule za Sekondari ili kumaliza changamoto ya upungufu wa walimu wilayani hapo.

Kauli hiyo imetolewa na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Pangani, Bw. Kaunga Kaunga wakati akizungumza na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC, Gerard Chami alipofika ofisini hapo hivi karibuni kwa lengo la kupata taarifa juu ya utekelezaji wa majukumu ya Tume hiyo wilayani hapo.

Kaunga alisema Wilaya hiyo ina jumla ya shule za msingi 32 na shule za sekondari nane (8) pamoja na shule shikizi saba (7) huku ikiwa na jumla ya walimu 357 ambapo katika idadi hiyo, walimu 211 ni wa shule za Msingi na 146 ni wa shule za sekondari.

Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Pangani, Bw. Kaunga Kaunga (wa kwanza kulia) akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi ya TSC Wilaya ya Pangani kwa Mkuu wa Kitengo cha Mawasilano ya Serikali wa TSC, Gerard Chami wakati Mkuu huyo wa Kitengo alipofanya ziara wilayani hapo hivi karibuni.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasilano ya Serikali wa TSC, Gerard Chami akizungumza na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Pangani, Bw. Kaunga Kaunga katika ofisi za TSC wilayani Pangani hivi karibuni.

"Walimu wetu wanajitahidi kufanya kazi kwa bidii katika kufundisha wanafunzi, lakini hawa tulionao bado hawajatosheleza tukilinganisha shule tulizonazo. Tulifanya tathmini tukaona kwamba tunahitaji walimu 87 wa shule za msingi na 17 wa shule za sekondari kwa masomo ya sayansi. Tunaamini kwa kadiri serikali itakavyoweza itaendelea kuongeza walimu ili kumaliza upungufu uliopo," alisema.

Akizungumzia kuhusu maendeleo ya walimu Kaunga alisema katika kipindi cha miaka

WALIMU 87 MSINGI, 17 SEKONDARI WAHITAJIKA KUMALIZA TATIZO LA UPUNGU WA WALIMU PANGANI

Picha ya pamoja kati ya Mkuu wa Kitengo cha Mawasilano ya Serikali wa TSC, Gerard Chami (katikati), Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Pangani, Bw. Kaunga Kaunga (kushoto) na Afisa wa TSC katika Ofisi ya TSC Pangani.

miwili, 2020/2021 na 2021/2022 TSC wilayani hapo ilipandisha vyeo walimu 74 katika madaraja mbalimbali ambapo walimu 44 ni wa shule za sekondari na 40 ni wa shule za msingi huku mwalimu mmoja (1) akibadilishiwa cheo baada ya kujiendeleza kielimu.

"Kazi ya kuwapandisha vyeo walimu na kuwabadilishia cheo baada ya kujiendeleza kielemu ni endelevu, kuna wakati anakuja mwalimu mmoja mmoja akiwa na tatizo maalum, hao nao tumeendelea kuwashughulikia kwa kushirikiana na mamlaka zingine. Hata sasa tuna walimu 29 wenye sifa za kubadilishiwa cheo ambao tunaendelea kuwashughulikia ili kukamilisha taratibu zao," alisema.

Kwa upande wa hali ya nidhamu kwa walimu, kiongozi huyo alisema kuwa walimu wameendelea kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria kanuni na taratibu na kufanya mashauri ya nidhamu kupungua ambapo katika kipindi cha kuanzia Julai 2019 hadi Septemba 2022 walimu saba (7) ndio waliofunguliwa mashauri ya nidhamu huku akieleza kuwa mafaniko hayo yanatoakana na elimu inayotolewa na Tume hiyo.

"Wakuu wa Shule wanajitahi kusimamia masuala ya nidhamu na maadili ya Walimu kama mamlaka ya kwanza ya nidhamu kwa mwalimu kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448. Hata hivyo, tunaona kuna changamoto ya baadhi yao kushindwa kuchukua hatua kwa makosa yaliyo kwenye mamlaka zao. Tunaendelea kuwaelimisha ili waweze kusimamia walimu kama inavyohitajika," alisema.

Kaunga alihitimisha kwa kueleza kuwa Ofisi ya TSC Pangani inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo upungufu wa vitendea kazi vya ofisi, upungufu wa watumishi ambapo kwa sasa ofisi hiyo ina watumishi wawili (2) pekee pamoja na kutokuwa na chombo cha usafiri kwa ajili ya kuwafikia walimu kwa wakati.

MNKANDE AELEZA MAFANIKIO YA TSC WILAYA YA MKINGA

Na Mwandishi Wetu – Mkinga.

Wilaya ya Mkinga ni moja kati ya Wilaya 8 za Mkoa wa Tanga na ina Tarafa mbili (2) zenye jumla ya Kata ishirini na mbili (22). Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mkinga inahudumia jumla ya Walimu 896 ambapo walimu 556 ni wa shule za msingi na 340 ni wa sekondari huku walimu hao wakiwa katika shule 82 za msingi na shule 15 za sekondari mtawalia.

Akizungumza na jarida hili hivi karibuni Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Mkinga, Thomas Mnkande alieleza kuwa katika mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya walimu 39 waliajiriwa na kusajiliwa ambapo walimu 19 ni wa shule za msingi na walimu 20 wakiwa ni wa shule za Sekondari.

Alibainisha kuwa moja ya majukumu yanayotekelezwa na ofisi yake ni kuthibitisha kazini walimu baada ya kukidhi vigezo wakati wa muda wa matazamio ambapo katika mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya walimu 88 walithibitishwa kazini, kati ya hao walimu 63 ni wa shule za msingi na walimu 25 ni wa shule za sekondari.

Kikao kati ya Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami (wa kwanza kulia) pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Mkinga kikiwa kinaendelea. Kikao hicho kimefanyika hivi karibuni katika ofisi za TSC wilayani Mkinga hivi karibuni.

Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Mkinga, Thomas Mnkande akifafanua taarifa ya utekelezaji wa ofisi hiyo wakati wa kikao cha watumishi wa ofisi hiyo na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC kilichofanyika hivi karibuni.

Kaimu Katibu Msaidizi huyo aliongeza kuwa katika mwaka wa fedha 2021/2022 walimu 173 walipandishwa vyeo ambapo katika idadi hiyo walimu 110 ni wa shule za msingi na 63 ni wa shule za Sekondari huku akiweka bayana kuwa zoezi hilo lilizingatia taratibu zote zinazohusika.

"Zoezi hili lilizingatia taratibu zote ikiwa ni pamoja na Mwajiri kuwasilisha orodha ya Walimu waliotengewa bajeti na waliopendekezwa kupandishwa vyeo kwenye Mamlaka ya ajira na nidhamu, Kamati ya Tume kufanya kikao cha kuwapandisha Walimu vyeo na kuwabadilisha kada Walimu waliojiendeleza, Tume kuwasilisha orodha ya waliopandishwa vyeo na kubadilishiwa kada kwa mwajiri pamoja na kuandaa barua za kuwapandisha vyeo na kuwabadilishia vyeo waliojiendeleza," alifafanua.

MNKANDE AELEZA MAFANIKIO YA TSC WILAYA YA MKINGA

Pamoja na hayo, katika mwaka wa fedha 2021/2022 TSC Wilaya ya Mkinga ilifanikiwa kuwabadilishia cheo walimu 78 baada ya kujiendeleza kielimu ambapo katika idadi hiyo walimu 62 ni wa shule za msingi na 16 wa shule za sekondari.

Kuhusu nidhamu kwa walimu, Mnkande anaeleza kuwa hali ya nidhamu ya walimu wilayani hapo inaendelea kuwa nzuri kwasababu ya mafunzo ya mara kwa mara yanayotolewa na Tume hiyo jambo ambalo limewafanya Walimu kuzingatia sheria na kanuni za Utumishi wa Walimu na hivyo kujiepusha na makosa mbalimbali ya kinidhamu.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami (kushoto) akizungumza wakati wa kikao kilichowahusisha watumishi wa TSC Wilaya ya Mkinga kilichofanyika katika ofisi za TSC Mkinga hivi karibuni.

"Katika kipindi cha kunzia mwaka wa fedha 2019/2020 hadi 2022/2023 tumekuwa na mashauri 38 ya walimu. Mwaka wa fedha 2019/2020 tulikuwa na mashauri 27, mwaka 2020/2021 mashauri sita (6), mwaka 2021/2022 mashauri 4 na mwaka huu 2022/2023 tumepokea shauri moja. Ukiangalia tulikotoka na tunakoelekea unaweza ukaona kuna kazi imefanyika na kumekuwa na mabadiliko kwa walimu wetu," alisema.

"Pamoja na mafanikio hayo ya kuimarika kwa nidhamu, lazima nikiri kuwa bado kuna baadhi ya Wakuu wa Shule ambao wanashindwa kusimamia na kutekeleza wajibu wao kama sheria inavyowataka kufanya. Pamoja na kwamba tumekuwa tukiwaelimisha mara kwa mara, tumegundua kuwa moja ya sababu za kushindwa kutekeleza wajibu wao ni hofu ya kulaumiwa na kuonekana wabaya kwa walimu wanaowachukulia hatua za sheria," Mnkande aliongeza.

Anahitimisha kwa kueleza kuwa ofisi yake inajivunia kwakuwa matatizo ya Walimu yameendelea kutatuliwa kwa haraka mara yanaporipotiwa na pia, walimu wanapapata uhuru wa kutosha kueleza changamoto zao.

Mmoja wa watumishi wa TSC Wilaya ya Mkinga akichangia hoja wakati wa kikao cha watumishi hao na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kilichofanyika katika ofisi za TSC wilayani Mkinga hivi karibuni.

Picha ya pamoja kati ya Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC, Gerard Chami (wa kwanza kutoka kushoto) na watumishi wa TSC Wilaya ya Mkinga.

Kaimu Katibu Msadizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Handeni, Elizabeth Chikira akizungumza na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami (hayupo pichani) katika ofisi za TSC Handeni hivi karibuni.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami (kulia) akizungumza na Kaimu Katibu Msadizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Handeni, Elizabeth Chikira katika ofisi za TSC Handeni hivi karibuni.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami (kulia) akimwonesha jambo Kaimu Katibu Msadizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Handeni, Elizabeth Chikira katika ofisi za TSC Handeni hivi karibuni.

TUNAHUDUMIA WALIMU 1356: TSC MUHEZA

Na Mwandishi Wetu – Muheza.

Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Muheza, Fatma Rajab alisema kuwa wilaya hiyo ina jumla ya Walimu wa Shule za Sekondari 576 ambapo wanaume ni 393 na wanawake ni 183 huku Walimu wa Shule za Msingi wakiwa ni 780 ambapo wanawake ni 407 na wanaume ni 373.

Fatma alieleza hayo hivi karibuni wakati alipotembelewa na Maafisa wa Kitengo cha Mawasilano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu kwa lengo la kupata taarifa juu ya namna ofisi hiyo inavyowahudumia walimu ambapo alieleza kuwa Wilaya hiyo ina jumla ya Shule 146 za Serikali zikiwemo Shule 113 za Msingi, Shule 33 na Sekondari na Shule Shikizi 04.

Akizungumzia utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo, Fatma alisema¬ kuwa Mwezi Julai 2022 ofisi yake ilipokea jumla ya walimu 46, ambapo walimu wa Shule za Msingi walikuwa 18 na walimu wa Shule za Sekondari walikuwa 28 ambapo ofisi hiyo ilifanya jukumu la kuwasajili na kuwapa barua za ajira kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448.

Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya Muheza, Fatuma Rajab akizungumza na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC, Gerard Chami (hayupo pichani) wilayani Muheza hivi karibuni.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC, Gerard Chami (kulia) akizungumza na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya Muheza, Fatuma Rajab katika ofisi za TSC Muheza hivi karibuni.

Kuhusu kupanda vyeo kwa walimu, Kaimu Katibu Msaidizi huyo alieleza kuwa katika mwaka wa Fedha 2021/2022 jumla ya Walimu 314 walipandishwa vyeo, kati ya hao walimu 217 ni wa Shule za Msingi na 67 walikuwa ni kutoka Shule za Sekondari huku walimu wawili (2) wakibadilishiwa cheo baada ya kujiendeleza

TUNAHUDUMIA WALIMU 1356: TSC MUHEZA

Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya Muheza, Fatuma Rajab akiwa anachukua dondoo wakati wa kikao chake na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC, Gerard Chami (hayupo pichani). Kikao hicho kilichofanyika hivi karibuni katika ofisi za TSC Muheza.

kielimu.

Alieleza kuwa katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia Julai 2019 hadi Juni 2022 Ofisi ya TSC Muheza imeshughulikia mashauri ya nidhamu 22 ambapo mwaka 2019/2020 kulikuwa na mashauri tisa (9), mwaka 2020/2021 mashauri sita (6) na mwaka 2021/2022 kulikuwa na mashauri saba (7).

"Katika mashauri 22 yaliyofunguliwa, mashauri 18 yalihusu utoro na mengine yalihusu uhusiano wa kimapenzi na mwanafunzi (1), kukiuka maadili ya kazi (1), kukataa uhamisho (1) na kughushi vyeti (1). Katika makosa hayo walimu 16 walifukuzwa kazi na walimu 6 walipewa adhabu nyingine zikiwemo kukatwa mshahara kwa 15% kwa muda wa miaka mitatu pamoja na onyo," Fatma alieleza.

Kaimu Katibu Msaidizi huyo alifafanua kuwa Mamlaka za Wakuu wa Shule katika Kusimamia Maadili ya Utumishi Walimu yanatekelezwa kwa ufanisi kwa vile wakuu wa shule wanasimamia ipasavyo majukumu yao kuakikisha walimu wanafanya kazi kwa bidii kwa kufuata Sheria na Kanuni za Utumishi wa Walimu, pia wamefanikiwa kuthibiti utoro kwa walimu.

"Ofisi ya TSC muheza inajivunia mambo mbalimbali kutoka kwa Walimu tunaowasimamia kwa kuwa asilimia kubwa wanazingatia sheria kanuni na taratibu katika kutekeleza majukum yao. Idadi ya makosa yanayotokana na Utoro yanapungua kwa kiasi kikubwa kila mwaka kwa vile Walimu wanaelimishwa kuhusu kuzingatia Miiko na Maadili ya kazi ya ualimu," alisema Fatma.

Akieleza kuhusu changamoto za walimu, Fatma alisema kuwa miongoni mwa hizo ni baadhi ya walimu kutokujiendeleza kitaaluma jambo ambalo linasababisha kukosa sifa za kupanda vyeo vya juu zaidi badala yake wanaishia kwenye vyeo vya ukomo, baadhi ya walimu kukopa bila kuwa na malengo sahihi ya fedha kitu kinachosabasha fedha za mkopo kuishia katika matumizi yasiyo na tija pamoja na baadhi ya walimu kukopa kupita kiasi jambo ambalo linasababisha kushindwa kutekeleza majukumu yao vizuri kutokana na usumbufu wa kudaiwa.

"Tunaendelea kutoa elimu ili kuhahakisha changamoto hizi zinamalizika na walimu wanafanya kazi wakiwa na amani na kuongeza tija katika kuwafundisha wanafunzi," alisema.

KATIBU NKWAMA AWAPA KONGOLE TIMU YA WANAMICHEZO TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)

Na Mwandishi Wetu – Dodoma.

Katibu wa Ofisi ya Rais – Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Mbena Nkwama, *ndc* amekipongeza kikosi cha wachezaji wa michezo mbalimbali wa Tume kwa kushiriki na kupata ushindi wakati wa Mashindano ya Kitaifa ya Michezo ya Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali Tanzania (SHIMIWI) iliyofanyika Mkoani Tanga hivi karibuni.

Ametoa pongezi hizo kwa wanamichezo hao walioshiriki kwenye michezo mbalimbali wakiwawakilisha wachezaji wengine wa Tume ikiwemo michezo ya mpira wa pete, karata, draft, mbio za baiskeli, riadha, darts na kurusha tufe mara baada ya kupokea vikombe viwili na medali mbili kutoka kwa Katibu wa Klabu ya Michezo ya Tume ya Utumishi wa Walimu *(TSC Sports Club),* Enid Geofrey Mwabulambo wakati wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume uliofanyika hivi karibuni.

Katibu Nkwama alitumia fursa hiyo pia kuwaasa wanamichezo wa Tume hiyo kuongeza juhudi zaidi katika kufanya mazoezi ili kuongeza kasi kwenye ushiriki wa michezo licha ya michezo kuwa ni ajira kwa wanamichezo wengine kwani pia inaleta afya na kujenga mahusino mazuri baina ya wanamichezo kutoka maeneo tofauti na ndani ya Serikali hivyo anaamini itaongeza ufanisi zaidi katika ufanyaji kazi.

"Licha ya kuwa michezo ni ajira lakini kwa wengine wanaoenda kwenye mashindano makubwa huwa kubwa zaidi ni kujenga afya, mahusiano na kupumnzisha mwili baada ya kazi kwakuwa huwezi kila siku kuwa ofisini tu unafanya kazi muda wote kwahiyo ni vizuri kuongeza ushiriki na wakati mwingine hali itakaporuhusu zaidi tutaweka ulazima wa watu kushiriki ili tuibue vipaji vingine zaidi vilivyojificha."alisema Katibu

Aidha Katibu amewataka viongozi wa Michezo wa Tume ya Utumishi wa Walimu kuhakikisha wanaongeza kasi zaidi katika kutafuta wadhamini wa michezo ambao kwa sehemu kubwa ni wadau wa Tume hapa nchini ikiwa ni pamoja na kudumisha utamaduni wa mazoezi ya kila mwisho wa wiki kutekeleza maelekezo ya Serikali kwa Watumishi wake ili

KATIBU NKWAMA AWAPA KONGOLE TIMU YA WANAMICHEZO TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)

kuendeleza michezo na washiriki wanapokwenda SHIMIWI na kwenye mashindano mengine waweze kurudi na vikombe vingi zaidi.

"Hata ikiwezekana pale hali ya fedha itakaporuhusu basi Tume Makao Makuu Dodoma na Ofisi zake Wilayani tuwe tunafanya mabonanza angalau mara moja au mbili kwa mwezi. Mimi na viongozi wengine wa Tume tutakuwa mstari wa mbele kuibeba na kuipeperusha bendera ya Tume, na tukifanya hivi kila mwezi visukari vitakimbia. Michezo ya aina hiyo inatufurahisha na huu utaratibu ukiendelezwa hata tukishiriki SHIMIWI tutarudi na vikombe vingi zaidi". Alisema

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Klabu ya Michezo Tume ya Utumishi wa Walimu, Ndg. Gerard Julius Chami, alisema licha ya mpambano kuwa mkali katika mashindano hayo, wanamichezo wote walioiwakilisha Tume walicheza na kupambana kwa kiwango kikubwa bila kukata tamaa licha ya baadhi ya michezo kutopata matokeo mazuri.

Michezo ya Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali Tanzania (SHIMIWI) ilifanyika Mkoani Tanga kuanzia tarehe 01 hadi 15 mwezi Oktoba, 2022 kwa kushirikisha wanamichezo kutoka Wizara na Taasisi mbalimbali ikiwemo Tume ya Utumishi wa Walimu iliyoshirikisha wanamichezo 13 na hivyo kuibuka Mshindi wa Pili na kupata Medali ya Silver katika mchezo wa Kurusha Tufe (Wanawake), Mshindi wa Tatu na kupata Kombe katika Mchezo wa Vishale (Darts kwa Wanawake), Mshindi wa Tatu na kupata Kombe katika Mchezo wa Draft (Wanawake), kuingia nafasi ya nusu fainali katika Mchezo wa Karata (Wanawake), kuingia fainali katika Mchezo wa Riadha Wazee (Wanawake) dhidi ya wapinzani Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kuingia nafasi ya nusu fainali katika Mchezo wa Riadha Wazee (Wanaume), kuingia nafasi ya fainali katika Mchezo wa Riadha Mita 100 (Wanawake), kuingia nafasi ya fainali katika Mchezo wa Riadha kupokezana vijiti (*Relay* Wanawake) dhidi ya wapinzani Wizara ya Uchukuzi na Usafirishaji na washindi wa 20 kati ya 38 katika Mchezo wa Mbio za Baiskeli Kilomita 45 (Wanaume).

HINDANO YA SHIMIWI 2022
AIFA TANGA 01-15/10/2022
KAULI MBIU
KAZI IENDELEE

GD

MASOUD COURT
GK

SHAMBA
Taifa

SWARA

agricom
agricom
agricom
kuongeza tija mahali pa

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 **Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz** **Tovuti: www.tsc.go.tz**

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania